Remove Watermark Now

# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

## OFISI YA RAIS

## TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

**RASIMU YA MPANGO NA BAJETI KWA MWAKA 2017/2018 KATIKA UTEKELEZAJI WA MPANGO WA II WA MAENDELEO WA TAIFA 2017/2018 – 2020/2021**

Mkurugenzi Mtendaji,
S.L.P 88,
**Ngudu.**
Barua pepe: dedkwimba@yahoo.com
Nujushi: 0732-980844
Simu: 0732-980528

Januari , 2017

Remove Watermark Now

# MAPENDEKEZO YA MPANGO NA BAJETI KWA MWAKA 2017/2018

1:0 **UTANGULIZI**

Mhe. Mwenyekiti,

Halmashauri ya Wilaya ya Kwimba ni miongoni mwa Halmashauri nane za mkoa wa mwanza na ni Halmashauri pekee ambayo haipitiwi na ziwa Victoria hivyo kupelekea kukosa vyanzo vinavyotokana na ziwa.Halmashauri inayo majimbo mawili ya Uchaguzi, Jimbo la Sumve na Jimbo la Kwimba. Kwa kutumia Sensa ya watu na makazi ya Mwaka 2012 idadi ya watu ni 406,509 wakiwemo wanawake 208,413 na wanaume 198,096 Kutokana na ongezeko la watu kwa mwaka kuwa 3% kwa mwaka 2016 kuishia mwezi Desemba Halmashauri in wastani wa wakazi wapatao 462,663.

Rasimu ya Mpango na Bajeti imezingatia mambo mbalimbali yakiwemo;

**A. MAMBO YA KISERA,**

- Mwongozo wa Uandaaji wa Mpango na Bajeti kwa mwaka 2017/2018 uliotolewa na Wizara ya Fedha na Mpango;
- Mpango wa II wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano 2016/17-2020/21;
- Sheria ya Bajeti Na 11 ya mwaka 2015 na Kanuni zake;
- Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2015;
- Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025 (TDV-2025);
- Mpango wa Maendeleo endelevu (SDGs);
- Maagizo na Maelekezo ya Mheshimiwa Rais kupitia hotuba yake ya ufunguzi wa Bunge la Jamhuri la Muungano wa Tanzania.
- Sera za kisekta na mipango shirikishi Jamii (O&OD).
- Maeneo mahsusi ikiwa ni pamoja na ukamilishaji wa miradi, ulipaji wa madeni, kujenga uwezo, ununuzi wa vifaa vya kuendeshea ofisi na masuala mtambuka kama vile huduma/ulinzi wa watoto (Child Protection), Utunzaji na hifadhi ya mazingira, uweezeshaji wananchi kiuchumi ikiwa ni pamoja na vikundi vya vijana na wanawake na gharama za kukabiliana na majanga.

**2:0 MAPITIO YA BAJETI YA 2016/2017 HADI DISEMBA 2016**

- Mhe. Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2016/2017 Halmashauri iliidhinishiwa kukusanya na kutumia jumla ya Tshs. **40,476,049,000.00** kati ya hizo Tshs. **29,876,686,000.00** ruzuku ya Mishahara, Tshs. **2,404,305,000.00** ni ruzuku ya matumizi

iskysoft

Remove Watermark Now

mengineyo, Tshs. **6,396,157,000.00** ni miradi ya maendeleo na **Tshs.1,798,901,000.00** ikiwa ni Mapato ya ndani.

- Mhe. Mwenyekiti, katika kipindi cha miezi sita (Julai 2016 – Dec 2016) Halmashauri imepokea kiasi cha Tshs. **19,253,349,784.03** sawa na asilimia **47.6** kama inavyoonekana katika jedwali hapa chini:
- **FEDHA ZILIZOIDHINISHWA NA KUPOKELEWA/KUKUSANYWA HADI DISEMBA 2016**

| Kasma | Maelezo ya Mapokezi ya Fedha | Makisio | Mapokezi Halisi | % |
|---|---|---|---|---|
| Halmashauri ya Wilaya ya Kwimba<br><br>(81-M2) | Mapato ya Ndani | 1,798,901,000.00. | 611,493,084.02 | 34 |
| | Mishahara | 29,876,686,000.00 | 14,282,455,25281 | 43 |
| | Matumizi Mengineyo | 2,404,305,000.00 | 592,823,600.00 | 25 |
| | Miradi ya Maendeleo | 6,396,157,000.00 | 3,256,667,634.16 | 24.65 |

iskysoft

**2.1 Makusanyo ya Mapato ya ndani hadi Desemba 2016**

Mhe. Mwenyekiti, katika kipindi cha miezi sita (Julai 2016 – Dec 2016) Halmashauri imefanikiwa kukusanya jumla ya **Tshs 611,493,084.02** kama jedwali linavyoonyesha.

| Kasma | Maelezo ya Mapokezi ya Fedha | Makisio | Mapokezi Halisi | % |
|---|---|---|---|---|
| Halmashauri ya Wilaya ya Kwimba<br><br>(81-M2) | 2.1 Mapato ya Ndani | 1,798,901,000.00. | 611,493,084.02 | 34 |

Remove Watermark Now

## 2.2 Makisio ya Matumizi na matumizi halisi hadi Desemba, 2016

Mhe. Mwenyekiti, katika kipindi cha miezi sita (Julai 2016 – Dec 2016) Halmashauri imetumia kiasi cha Tshs. **20,522,800,157.76** sawa na asilimia **50.7** kama jedwali linavyoonekana hapo chini:-

| Chanzo cha Fedha | Aina ya Matumizi | Makisio | Matumizi | % |
|---|---|---|---|---|
| | | | | |
| Mapato ya Ndani | Mishahara | 3,924,000.00 | 1,156,556.80 | 29.5 |
| | Matumizi Mengineyo | 719,791,000.06 | 338,086,726.05 | 47 |
| | Miradi ya Maendeleo | 1,074,947,999.94 | 85,488,871.51 | 7.95 |
| Ruzuku ya PE & OC | Ruzuku ya Mishahara | 29,876,686,000.00 | 14,282,455,252.81 | 47.8 |
| | Matumizi Mengineyo | 2,404,305,000.00 | 2,808,108,476.73 | 116.8 |
| Ruzuku Miradi ya Maendeleo | Miradi ya Maendeleo fedha za ndani | 2,361,515,000.00 | 43,921,000.00 | 1.86 |
| | Miradi ya Maendeleo fedha za nje | 4,049,462,000.00 | 2,328,286,073.86 | 98.2 |
| | **Jumla kuu** | **40,476,049,000.00** | **19,887,502,957.76** | **49.13** |

iSkysoft

## 2.3 MAFANIKIO

- Tumefanikiwa kununua mashine maalumu 20 za kukusanyia mapato (POS) na tayari zimeanza kutumika katika kata 20 za Jimbo la Kwimba na Sumve.
- Tumefanikiwa kuunda task force ya kufutilia mapato inayofanya kazi ya kukusanya mapato kwa kila chanzo.
- Ongezeko la ushuru wa mazao kutoka Tshs 1000 hadi Tshs 4000, kuongezeka kwa mavuno ya zao la dengu na udhibiti wa utoroshaji wa mazao pia imesaidia kuongeza mapato yatokanayo na vyanzo vya ndani vya Halmashauri ambapo mpaka kufikia Disemba 2016 tumefanikiwa kukusanya kiasi cha **Tshs 201,111,086.50** sawa na **asilimia 86** ya makisio ya mwaka kutoka katika chanzo hiki
- Ushiriki mkubwa kutoka kwa kamati ya Ulinzi na usalama umeongeza uelewa wa wananchi juu ya umuhimu wa ulipaji kodi .

.

Remove Watermark Now

## 2.4 CHANGAMOTO NA MIKAKATI YA KUKABILIANA NAZO

**CHANGAMOTO**

Mheshimiwa Mwenyekiti,

Katika kutekeleza bajeti ya 2016/2017 Halmashauri imekabiliwa na changamoto zifuatazo:-

i) Utekelezaji wa agizo la kutenga asilimia 60 ya mapato ya ndani kwenye miradi ya maendeleo ni kitu ambacho kihalisia hakiwezekani kwani baada ya Halmashauri kutenga asilimia hii na asilimia kumi ya wanawake na vijana hubakiwa na asilimia 30 tu ambayo katika hiyo asilimia 20 ni ya Vijiji, asilimia 5 kuchangia miradi ya wafadhiri, hivyo tunabakiwa na asilimia 5 kuendesha Ofisi idara za zisizo pata ruzuku, kulipa vikao vya kisheria na posho ya mwezi ya Waheshimwa Madiwani.

ii) Upungufu wa Watumishi katika idara mbalimbali hivyo kupelekea utoaji wa huduma kwa Umma usioridhisha;

iii) Kuchelewa kupokelewa kwa fedha za matumizi mengineyo na Miradi ya maendeleo kutoka Serikali Kuu, hivyo kuathiri utoaji wa huduma kwa jamii na utendaji wa kazi za Halmashauri;

iSkysoft

iv) Hamasa ndogo ya jamii katika kuchangia miradi ya maendeleo

v) Gharama kubwa ya Pembejeo hasa madawa iliyosababisha wakulima kushindwa kulima/kuhudumia zao la pamba ambalo ni chanzo kikubwa mapato ya ndani kwa Halmashauri;

vi) Baadhi ya makampuni ya pamba kukwepa kulipa ushuru;

vii) Wakulima kususia kulima zao la pamba ambalo ni chanzo kikubwa cha mapato Kwimba kutokana na bei ndogo;

viii) Mabadiliko ya hali ya hewa yanayosabisha kuwa na mvua nyingi kwa kipindi kifupi na jua la muda mrefu hivyo kuathiri upatikanaji wa mazao mchanganyiko ambacho ni chanzo cha pili cha mapato ya Halmashauri;

ix) Mkanganyiko wa Sheria ya "Hotel levy Act", sura ya 105 iliyofutwa na Sheria ya Utalii Na.29 ya mwaka 2008 hufanya baadhi ya wafanyabiashara kugoma kulipa *hotel levy.*

x) Mkanganyiko kuhusu namna ya ukusanyaji wa kodi ya majengo (Property tax).

xi) Uelewa mdogo wa wananchi kuhusu kulipa ushuru na tozo mbalimbali;

xii) Udanganyifu wa wafanyabishara wa mazao katika kulipa ushuru na wakati mwingine kutoroka nyakati za usiku bila kulipa ushuru.

xiii) Kutotolewa kabisa kwa fedha za miradi ya Maendeleo mfano Ruzuku ya maendeleo ya Serikali za Mitaa haikupokelewa mwaka huu.Matokeo yake ni kutokukamilika kwa miardi mingi ya maendeleo katika sekya za Elimu, Afya na mifugo na kilimo;

xiv) Kuchelewa kwa fedha za miradi hasa miradi ya barabara;

Remove Watermark Now

xv) Kukosekana kwa fedha za uendeshaji wa ofisi na hivyo Halmashauri kuwa na madeni makubwa ya watoa huduma wa mafuta, shajala, matengenezo ya magari, ununuzi wa matairi, umeme , maji na haki za watumishi kama likizo, fedha za kujikimu, matibabu na stahili za Wakuu wa Idara.

xvi) Uchangiaji mdogo wa wananchi katika shughuli za maendeleo;

xvii) Uharibifu mkubwa wa mazingira unaotokana na kukata miti hovyo na uchungaji wa makundi makubwa ya ng’ombe;

xviii) Upungufu wa watumishi hasa katika sekta za Afya, Elimu(walimu wa masomo ya sayansi na hisabati), Kilimo na Mifugo kunakopelekea utoaji hafifu wa huduma katika sekta hizo;

xix) Mazingira magumu ya kufanyia kazi kutokana ukosefu/upungufu wa ofisi na nyumba za watumishi hasa maeneo ya Vijijini

## 3.0 MPANGO NA BAJETI KWA MWAKA 2017/2018

## 3.1 VIPAUMBELE VYA HALMASHAURI KATIKA MWAKA 2017/2018

### i. Sekta za Kiuchumi

- Ujenzi wa stendi ya mabasi na kituo cha kuegesha magari makubwa; katika mji wa Biashara wa Hungumalwa katika barabara ya kuelekea Shinyanga ili kuongeza mapato ya Halmashauri;
- Ukamilishaji wa Kantini ya Halmashauri ili kuweza kuongeza mapato.
- Kuimarisha na kuboresha miundombinu ya masoko ya mifugo na mazao yake kwa kujenga uzio katika mnada wa Bungulwa ili kuzuia wakwepa kodi na ushuru.
- Kuimarisha upimaji endelevu wa mpango bora wa matumizi ya ardhi, uthamini, na upimaji wa maeneo ya taasisi za Serikali na maeneo ya masoko na Ujenzi wa Masjala ya Ardhi;
- Upandaji wa Miti kwenye taasisi za Umma, binafsi na katika kaya;
- Kuongeza thamani ya mazao ya Alizeti, Mpunga Dengu na choroko ili kuongeza tija kwa wakulima;
- Ukamilishaji wa Skimu, mifereji ikiwemo miundombinu ya mashambani katika skimu za Umwagiliaji za Mahiga na Shilanona ili kuongeza uzalishaji wa mazao ya biashara na chakula;
- Kuendeleza upandikiza wa vifaranga vya samaki katika skimu ya Mahiga;
- Kutoa mafunzo kwa vyama vya Ushirika SACCOS na Ifugonho.
- Matengezo ya Barabara na ujenzi wa Madaraja/Karavati na kufungua barabara mkakati za kiuchumi na Kijamii
- Kutoa mikopo kwa wanawake na vijana walioko katika miradi midogo midogo ya kupunguza umaskini na kuongeza kipato.

iSkysoft

### ii. Sekta za Kijamii

Remove Watermark Now

- Ukamilishaji wa miradi viporo katika sekta za Elimu, Maji, Afya na miradi iliyoanzishwa na jamii;
- Utengenezaji wa madawati na ujenzi wa Vyoo Shule za Msingi na Sekondari;
- Uboreshaji wa Usafi na Mazingira katika Wilaya kwa kujenga vizimba vya taka.
- Kuboresha huduma kwa makundi maalum ya wazee, vijana, wanawake, Watoto waishio katika mazingira hatarishi, wajane na wagane na
- Kuendelea kuelimisha jamii juu ya kujikinga dhidi ya UKIMWI;

**iii. Utawala Bora**

- Kudumisha amani na utulivu ;
- Uboreshaji wa Maslahi ya Watumishi;
- Kuimarisha teknolojia ,habari na mawasiliano;
- Uimarishaji wa Mabaraza ya Ardhi ya kata na Wilaya.

**JEDWALI LA VIPAUMBELE VYA MPANGO NA BAJETI YA HALMASHAURI YA WILAYA YA KWIMBA MWAKA 2017/2018**

iSkysoft

| NA | SEKTA | ENEO KIPAUMBELE |
|---|---|---|
| 1 | Elimu Msingi (Msingi na Sekondari). | • Ujenzi/ukamilishaji wa miundombinu ya elimu: Vyumba vya madarasa, nyumba za walimu, vyoo, maabara, mabweni, mabwalo na ofisi. |
| 2 | Afya | • Ujenzi na uboreshaji wa miundombinu ya kutolea huduma za Afya: Zahanati, Wodi, Hospitali,vituo vya Afya na nyumba za watumishi wa Afya. |
| 3 | Maji | • Uimarishaji, uboreshaji na usambazaji wa huduma za maji: Ukamilishaji ujenzi wa Matanki ya maji, Ujenzi wa vituo vya kuchotea maji, upanuzi wa mtandao wa maji ya bomba (Mamlaka ya Mji- Ngudu).<br>• Uundaji, usajili na uimarishaji wa vyombo vya watumia maji.<br>• Usimamizi na uhifadhi wa vyanzo vya maji.<br>• Kuimarisha ukusanyaji wa mapato na kudhibiti matumizi mabaya ya fedha na rasilimali nyinginezo. |
| 4 | Fedha na Utawala | • Kuongeza vyanzo vya mapato kwa kuanzisha vyanzo vya mapato.<br>• Kuimarisha ukusanyaji wa mapato na kudhibiti matumizi ya mapato.<br>• Kuboresha na kuimarisha miundombinu ya mapato (Mifumo ya ukusanyaji mapato na vitendea kazi vingine vya Ofisi). |

Remove Watermark Now

| | | |
|---|---|---|
| 5 | Kilimo, Mifugo na Uvuvi | Kuboresha sekta za uzalishaji kwa kuimarisha miundombinu ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi kwa:<br><br>• Kuimarisha miundombinu ya umwagiliaji (Skimu ya Mahiga na Shilanona).<br>• Kuimarisha uzalishaji wa mazao ya chakula na bishara (Pamba, Alizeti, Dengu, Mahindi, Choroko na Mtama,).<br>• Ujenzi wa machinjio na ukamilishaji wa maabara ya mifugo.<br>• Upandikizaji wa vifaranga vya samaki katika bwawa la Mahiga.<br>• Kuimarisha kituo cha malisho ya mifugo (Feed Lot) Nyambiti kwa kutandaza mabomba ya maji, kujenga banio la mifugo na uzio. |
| 6 | Barabara | Kuboresha na uimarisha mtandao wa barabara za Halmashauri ya Wilaya ya Kwimba. |
| 7 | Ardhi na Mipango miji | Kuimarisha na kuboresha makazi kwa:<br><br>• Kuweka Mpango wa matumizi bora ya Ardhi (Upimaji wa maeneo na utoaji wa hati miliki).<br>• Utoaji wa Fidia.<br>• Kushughulikia migogoro ya Ardhi. |
| 8 | Maliasili na misitu | Kuimarisha, kuboresha, kutunza na kuhifadhi maliasili:<br><br>• Uhifadhi wa mazingira kwa kupanda miti.<br>• Utengenezaji/ununuzi wa mizinga ya nyuki ya kisasa. |
| 9 | Utumishi na Utawala | Kuzingatia utawala bora kwa kuimarisha na kutoa huduma kwa wananchi:<br><br>• Kuimarisha na kutoa maslahi ya watumishi.<br>• Kusimamia utoaji wa huduma kwa wananchi kwa kuzingatia mkataba wa huduma kwa mteja.<br>• Kusimamia taaluma na weledi wa watumishikatika utoaji huduma.<br>• Kusimamia mfuko wa kujenga uwezo wa watumishi na viongozi (Madiwani) kuhusiana na masuala mbalimbali ya uendeshaji wa Taasisi 8YA kitaaluma (Career).<br>• Ujenzi wa Ofisi za watendaji wa kata na vijiji.<br>• Mafunzo kwa watendaji na viongozi wa kuchaguliwa |
| 10 | Maendeleo ya Jamii | Kuwezesha wananchi kiuchumi na kijamii:<br><br>• Kuwezesha vijana na wanawake kiuchumi na kijamii.<br>• Kuwezesha wananchi kiuchumi.<br>• Kuielimisha jamii dhidi ya majanga na namna ya kayaepuka au kupunguza madhara yake.<br>• Kuhamasisha ushiriki wa jamii katika shughuli za maendeleo na masuala mtambuka. |

iSkysoft

Remove Watermark Now

| | | |
|---|---|---|
| 11 | Mipango, Takwimu na Ufuatiliaji | • Kuimarisha ukusanyaji na utumizaji wa takwimu.<br>• Kuhuisha Mpango Mkakati wa Halmashauri.<br>• Kuhuisha Mipango Shirikishi jamii ya Fursa na Vikwazo vya Maendeleo (Opportunity and Obstacle to Development-O&OD).<br>• Kuimarisha ufuatiliaji na tathmini ya miradi ya Maendeleo.<br>• Kuboresha uandishi wa taarifa za miradi.<br>• Kuandika maandiko mbalimbali ya miradi. |

**Note:** Baadhi ya vipaumbele hivi vipo katika randama ya bajeti (Kama kitabu cha Mpango na Bajeti 2017/2018) kulingana na ukomo wa Bajeti. Aidha baadhi ya miradi hasa ya sekta za uzalishaji imeandikiwa maandiko kwa ajili ya kupata ufadhili/nyongeza ya bajeti kutoka Serikali kuu na wadau wengine wa Maendeleo.

## 3.2 MAKADIRIO YA MPANGO NA BAJETI MWAKA 2017/2018

**Mheshimiwa Mwenyekiti,**

Kutokana na Sera mbalimbali za Serikali pamoja na Vipaumbele vya Halmashauri vilivyoelekezwa hapo juu. Halmashauri ya Wilaya ya Kwimba katika kipindi cha mwaka 2017/2018 inatarajia kukusanya na kutumia jumla ya Tshs. **51,490,734,144.00** kutoka katika vyanzo mbalimbali ikiwa ni ongezeko la wastani wa asilimia 26.97. kama Jedwali linavyoonekana hapa chini.

iskysoft

**Muhtasari wa Makadirio ya Mpango na Bajeti 2016/2017 na 2017/2018**

| **Kasma** | **Maelezo ya Mapokezi ya Fedha** | **Makisio 2016/2017** | **Makisio 2017/2018** | **% ya Ongezeko** |
|---|---|---|---|---|
| Halmashauri ya Wilaya ya Kwimba<br><br>(81-M2) | Mapato ya Ndani | 1,798,901,000.00 | 2,100,000,000.00 | 11.18 |
| | Mishahara | 29,876,686,000.00 | 35,379,293,900.00 | 18.42 |
| | Matumizi mengineyo | 2,404,305,000.00 | 2,404,305,000.00 | 0 |
| | Miradi ya maendeleo | 6,396,157,000.00 | 11,607,135,244.00 | 81.47 |
| | **JUMLA KUU** | **40,476,049,000.00** | **51,490,734,144.00** | **26.97** |

## 3.3 MAKISIO YA MAKUSANYO YA NDANI MWAKA 2017/2018 NA MGAWANYO WAKE WA 60%- MIRADI YA MAENDELEO (DEV.) NA MATUMIZI MENGINEYO (OC)

Remove Watermark Now

**Mhe. Mwenyekiti ,**

Hlamashauri ya Wilaya ya Kwimba imetengewa kukusanya na kutumia jumla ya Tsh. 2,100,000,000.00 kutokana na vyanzo vya ndani. Asilimia 60 ya makisio hayo ni Tsh. 1,260,000,000.00 fedha hii itatumika kutekeleza miradi ya maendeleo. Na Asilimia 40 ni Tsh. 840,000,000.00. Fedha hizi zitatumika kwa matumizi mengineyo.

JEDWALI LA MIRADI YA KISEKTAITAKAYOTEKELZWA KWA VYANZO VYA NDANI 2017/2018

| NA | SEKTA | JINA LA MRADI | KIASI(TSH) |
|---|---|---|---|
| 1 | Maji | Uchimbaji wa kisima(Bore hole) katika kijiji cha Mwashilalage na Mwandu | 46,000,000.00 |
| 2 | Kilimo | Ujenzi wa banda la Nanenane, banda la wanayama kazi Malya, uanzishaji wa mashamba darasa ya pamba 20, Alizeti 10 katika tarafa 5; ukarabati wa skimu ya mahiga na Shilanona | 134,246,700.00 |
| 3 | Mifugo | Ukarabati wa majosho2 (Kiliwi na Nyashana), Ujenzi wa machinjio 2(Maligisu na Bupamwa), Upigaji chapa mifugo katika kata 30, na mafunzo kwa maafisa ugani wa mifugo katika uhamilishaji | 42,863,200.00 |
| 4 | Utawala | Kuwezesha ununuzi wa vifaa vya ukumbi (Retooling), Ununuzi wa POS (Point of Sells) 129 | 133,856,000.00 |
| | | | |
| 5 | Mipango Takwimu na Ufuatiliaji | Ujenzi wa Stendi ya mabasi katika kijiji cha Hungumalwa, Ufuatiliaji wa miradi ya kila mwezi na kila Robo, Uratibu na uendeshaji wa kamati ya Lishe wilayani. | 205,088,905.00 |
| 6 | Ardhi na Mipango miji | Kuwezesha uthamini katika kata 6(Malya, Nyambiti, Ngudu, Sumve na Hungumalwa); Kuwezesha upimaji wa viwanja katika eneo la Sumve na Hungumalwa); Kuwezesha upangaji wa Mji katika vijiji vya Runele, Mwagi na Mhande; na kuwezesha utoaji wa hati miliki za kimila katika vijiji 6. | 98,595,995.00 |
| 7 | Afya | Kuwezesha ukamilishaji wa zahanati za Kilyaboya, Sangu,Mwangika,Kishili, Mwamajila na Nyamatala | 200,000,000.00 |
| 8 | Maliasili | Kuwezesha upandaji wa miti 3,000,000 katika kata 30 | 20,000,000.00 |
| 9 | Maendeleo ya Jamii | Kuwezesha miradi ya Maendeleo ya vikundi vya vijana na wananwake katika kata 30. Kuwezesha uchangiaji wa mfuko wa vijana ( Youth Project through Sengerema foundation), Kuwwezesha kukabiliana na majanga na kuwezesha upatikanaji wa huduma kwa watoto (Children Protection) | 498,383,800.00 |
| 10 | Fedha na utawala | Ununuzi wa pikipiki za maafisa watenfdaji wa kata 5( Mhande, Maligisu,Kikubiji, Fukalo, Nyambiti na Bupamwa) kwa ajili ya kusaidia kukusanya mapato | 10,000,000 |
| | | **Jumla vyanzo vya ndani** | **1,389,850.00** |

iskysoft

JEDWALI LA MIRADI YA KISEKTA ITAKAYOTEKELZWA KWA
MBALIMBALI 2017/2018

Remove Watermark Now

| NA | SEKTA | JINA LA MRADI | KIASI(TSH) |
|---|---|---|---|
| | Mipango Takwimu na Ufuatiliaji | Ujenzi wa Stendi ya mabasi katika kijiji cha Hungumalwa, Ukamilishaji wa kantini, Ujenzi wa vibanda 5 katika Soko jipya la Ngudu, Utambuzi wa nguvu za Wananchi katika uzalishaji na shughuli za maendeleo, kuwezesha mikutano ya hamasa katika uwezeshaji wananchi kiuchumi katika vijiji 30, kuwezesha wananchi kiuchumi kwa kuwaunganisha na taasisi za kifedha na kiuchumi; kuwezesha uundaji wa mpango mkakati wa halmashauri 2016/17-2020/2021; kuwezesha watendaji wa kata 30 na vijiji 119 na maafisa ugani 15 katika utambuzi wa fursa na vikwazo na kuhisha mipango yao kwa mfumo wa (O&OD); kuwezesha uandaaji wa mipango na bajeti 2018/2019, kuwezesha kazi za LAAC, Uandaaji na utoaji taarifa za kila Robo (RS na kamati za Kudumu), kuwezesha mkaguzi wa ndani kukagua miradi kila robo na kuwesesha zoezi la Tathmini ya utendaji wa Halmashauri (Annual Assessment 2016/2017); ukusanyaji, uchambuzi na utunzaji wa takwimu katika kata5 na vijiji 60; kuwezesha maadalizi ya maandiko 10 kutoka katika idara 5 za Halmashauri; kuwezesha WEOs 30 kuandaa taarifa za miradi na kuziwasilisha katika mamalaka zinazohusika. | 326,361,995.00 |
| 2 | | | |
| 1 | | | |
| 2 | | | |
| | | | |
| 3 | | | |
| 4 | | | |
| | | | |
| 5 | | | |
| 6 | | | |
| 7 | | | |
| 8 | | | |
| 9 | | | |
| 10 | | | |
| | | | |
| | | | |

Remove Watermark Now

## 3.4 MIKAKATI YA KUONGEZA MAPATO

Kuendelea kubuni vyanzo vipya vya mapato na kuimarisha usimamizi wa ukusanyaji mapato kwa kutumia mfumo wa Ukusanyaji mapato kwa njia ya (Electronic);

- Kukamilisha taratibu za kupitishwa sheria ya ulipaji kodi za majengo ili kuwezesha Halmashauri kukusanya kodi za majengo;
- Kudhibiti utoroshaji wa mazao nyakati za usiku kwa kuweka vizuizi katika njia kuu za Nkalalo, Malya, Sumve, Ilula, Kikubiji na Bupamwa.
- Kuandika maandiko mbalimbali na kuyauza kwa wadau wa maendeleo ili kuongeza fedha za utekelezaji wa miradi ya maendeleo;
- Kuendelea kuomba kibali cha kuajiri watumishi kufuatana na ikama ili kupunguza tatizo la upungufu wa watumishi;
- Kuimarisha usimamizi na ufuatiliaji wa shughuli za maendeleo ili kupata ubora wa miradi na thamani ya fedha iliyotumika;
- Kuendelea kutoa elimu kwa jamii umuhimu wa kuchangia shughuli za maendeleo katika maeneo yao;
- Kuendelea kuelimisha jamii kuhusu suala la utunzaji wa mazingira.

iSkysoft

## 3.5 MAOMBI MAALUM

Pamoja na ukomo wa bajeti 2017/2018, Halmashauri inaomba kuongezewa fedha kiasi cha Tsh. 2,025,000,000.00 kwa ajili ya miradi ifuatayo:

- Ujenzi wa stendi ya mabasi ya Hungumalwa Tsh. 300,000,000.00;
- Ununuzi gari Idara ya Mipango kwa ajili ya ufuatilaji wa miradi ya maendeleo. Tsh. 75,000,000.00; Gari Idara ya Ardhi Tsh. 75,000,000.00 kwa ajili ya shughuli za Ardhi na Mipango miji na Gari la Idara ya Fedha Tsh. 75,000,000.00 kwa ajili ya ufuatiliaji wa mapato.
- Ujenzi wa vibanda Soko jipya la Ngudu Tsh. 100,000,000.00
- Fidia ya Ardhi/Viwanja kwa ajili ya Upangaji wa miji Tsh. 200,000,000.00
- Ujenzi wa Nyumba za Watumishi makao Makuu ya Halmashauri Tsh. 300,000,000.00;
- Ukamilishaji wa maabara Tsh. 600,000,000.00

Ongezeko hili la bajeti ikilinganiswa na mwaka 2016/2017 limetokana na

Remove Watermark Now

- Ongezeko la mishahara tokana na ajira mpya katika idara za Elimu, Afya,Kilimo na utawala, pia katika kumekuwapo na ongezeko la miradi ya maendeleo kutokana na kuingizwa kwa Miradi ya TASAF na Maji Vijijini.
- Halmashauri inatarajia kutekeleza miradi mbalimbali kisekta kutokana na vyanzo mbalimbali vya fedha za ndani na nje kama jedwali Na. 6 linavyoonesha.

**Jedwali Na. 6 Mgawanyo wa fedha za miradi za nje na za ndani Kisekta 2017/2018**

| Na | Maelezo | NDANI | NJE |
|---|---|---|---|
| 1. | TASAF | | 2,573,231,485.00 |
| 2. | Mfuko wa Barabara (R/F) | 1,064,590,000.00 | |
| 2 | Ruzuku ya Maendeleo (CBG) | 146,307,500.00 | |
| 3 | Ruzuku ya Maendeleo (CDG) | 1,316,767,500.00 | |
| 4 | SEDP | | 544,000,002.00 |
| 5 | Maji vijijini (RWSSP) | | 4,448,741,757.00 |
| 6 | Mfuko wa maendeleo ya Jimbo | 83,440,000.00 | |
| 8 | Ruzuku Maalum | 500,000,000.00 | |
| 9 | Mfuko wa Pamoja wa Afya (B/F) | | 930,057,000.00 |
| | **Jumla Kuu Fedha za Miradi ya Maendeleo za Ndani na Nje** | **3,111,105,000.00** | **8,496,030,244.00** |

iSkysoft

## 5.0: MIRADI INAYOOMBEWA KUINGIA KWENYE MPANGO WA MAENDELEO WA TAIFA WA MIAKA 5 AWAMU YA PILI.

Katika kushughulikia masuala mengine Muhimu, Halmashauri ya Wilaya ya Kwimba imeandaa na kuwasilisha Miradi ambayo imependekezwa kuwekwa kwenye awamu ya pili ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano. Miradi hii ina gharama za shilingi za Kitanzania **67,858,311,749.00** kama jedwali na. 7 linavyoonesha:- (Mhe. Mwenyekiti Naomba Wakuu wa Idara wawasilishe miradi ya Sekta zao).

**Miradi inayoombewa kuingizwa katika Mpango wa II wa Taifa wa Miaka Mitano 2016/2017-2020/2021**

| Na | Maelezo ya Mradi | Kiasi |
|---|---|---|
| 1. | Ujenzi wa stendi ya mabasi katika Mji wa Hungumalwa | 1,884,830,000.00 |
| 2.. | Ukamilishaji wa ujenzi wa skimu ya umwagiliaji katika kijiji cha Shilanona | 969,941,945.00 |
| 3. | Ukamilishaji wa skimu ya umwagiliaji katika kijiji cha | 1,486,200,000.00 |

| | | |
|---|---|---|
| | Mahiga | |
| 4. | Upanuzi wa mtandao wa kusambaza maji Ngudu Mjini | 2,000,000,000.00 |
| 5. | Ujenzi wa nyumba za walimu na madarasa katika shule za Sekondari | 2,354,308,000.00 |
| 6 | Ujenzi wa nyumba za walimu na madarasa katika shule za Msingi | 3,708,616,000.00 |
| 7 | Uimarishaji wa Minada ya Mifugo | 788,536,000.00 |
| 8 | Ujenzi wa chuo cha VETA- Ngudu | 1,668,336,870.00 |
| 9 | Maji Vijijini | 52,197,542,934.00 |
| 10 | Ujenzi wa masjala ya Ardhi | 300,000,000.00 |
| 11 | Ujenzi wa ofisi za watendaji na Vijiji na Kata | 500,000,000.00 |
| 12 | Uongezaji wa madawati | 1,000,000,000.00 |
| 13 | Ujenzi wa miundombinu ya Afya Vijijini(Zahanati na Vituo vya Afya) | 1,000,000,000.00 |
| 14 | Ujenzi wa miundombinu ya Barabara vijijini | 1,000,000,000.00 |
| | **JUMLA** | **70,858,311,749.00** |

Mhe. Mwenyekiti,

Naomba kuwasilisha.

Pendo A. Malabeja
**MKURUGENZI MTENDAJI**
**HALMASHAURI YA WILAYA KWIMBA.**

Remove Watermark Now
iSkysoft